**1013/1**
**KISWAHILI**
**MWIGO**
**KARATASI YA 1**
**MACHI 2019**
**MUDA: SAA 2**

**MWIGO**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**SAA 2**

***MAAGIZO:***

***a)*** *Mtihani huu una sehemu* ***NNE*** *muhimu;* ***Insha, Ufahamu****,* ***Matumizi ya Lugha*** *na* ***Sajili ya Lugha.***
*b) Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzoni mwa kila sehemu.*
*c) Andika majibu yako kwenye nafasi ulizoachiwa.*
*d) Usitoe karatasi yoyote katika kijitabu hiki.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

| SEHEMU | SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 20 | |
| 2 | 2 | 20 | |
| 3 | 3 | 30 | |
| 4 | 4 | 20 | |
| | 5 | 10 | |
| JUMLA | | 100 | |

***Karatasi hii ina kurasa 11 zilizopigwa chapa sawasawa. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.***

1. Andika insha isiyopungua maneno 350 kuhusu mojawapo ya;
   (a) Kama mkurugenzi wa Baraza la kitaifa la Lugha nchini Kenya, ni hatua zipi ungechukua kuimarisha ufasaha wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wananchi?

   (b) Wewe ni mwanachama wa klabu ya Kiswahili chuoni. Katibu wenu amekosa kuhudhuria mkutano na ametuma udhuru wa dharura. Wewe umeteuliwa kushikilia nafasi yake. Andika kumbukumbu za mkutano huo.

   (c) Andika insha kuhusu methali ifuatayo, “Muungwana akivuliwa nguo huchutama”

   (d) Endeleza; Naikumbuka siku hiyo vizuri sana, sijawahi kufedheheka jinsi ile maishani mwangu………………………

**SEHEMU YA PILI: UFAHAMU (ALAMA 20)**

2. ***Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.***

Siku moja, nilienda kumuona babu yangu kule kijijini bila kumtolea taarifa mbeleni. Nilipofika, nilimkuta amevaa **Magwanda yake yaliyokula chumvi hadi yakakinai.** Alinitazama huku akitabasamu na kusema, "Tabia hii yakuja kwangu bila taarifa utaikoma. Ukiendelea hivi utakuja **kwenda kwa wakwe wako upate ndio wanakwenda uchi**".

Kauli hii ya babu ilifanya nicheke. Tulisalimiana huku **tukipigiana pambaja.** Harufu ya manukato niliyojirashia asubuhi hiyo ilikutana na harufu ya jasho lake. Baadaye tuliingia ndani ya nyumba tukaketi **kwenye makochi yaliyoonyesha dalili za kuchoka**. Baada ya kuulizana habari za kimsingi, nilitaka kujua alikokuwa nyangya.

"Nyanyako ameenda kumuona jirani yetu mgonjwa. Amepata ajali akitoka mjini alikokuwa ameenda kuwatembelea wajukuu wake. **Raha yote ya kuwaona iligeuka karaha".** Alinyamaza kidogo, akaguna, kisha akaendelea, "Barabara hizi, sijui mwaziita, 'haiwei' zimewala watu wetu. Huwezi kuwahesabu kwa vidole tena".

Kwa muda, nilikosa la kusema. Niliona niubadili mkondo wa mazungumzo. Nilianza kwa kumweleza kuwa mazingira ya kijijini yalipendeza. Kwa kweli mandhari yale ya kijani hadi upeo wa macho yalisisimua sana. Sauti za ndege zilikuwa mfano wa muziki wa chini uliochezwa ili kuyapamba mazungumzo yetu. Mara kwa mara nilitekwa na sarakasi ya jogoo aliyetanua mabawa yake na kukaribia kuzungumza utadhani ni sauti ya mwanadamu. Nilipokuwa namtazama, nilishtuka mkono wa babu ulipoushika wangu, akaniongoza nje akisema, "Haina haja ya kuyamezameza mate. Huyu jogoo ni wako, leo tutamfanya kitoweo kwa ajili yako. Najua kule mjini mnakula kuku wa miigizo tu. Faida yao kwa mwili ni duni."

Tulishirikiana kumkamata Yule jogoo lakini baada ya muda, nilichoka. Moyo wangu ulikuwa unapiga kwa nguvu ajabu. **Niliona kisunzi**, nikakaa. Nikiwa najipumzisha chini ya kivuli cha mpera, nilisikia sauti za watoto waliokuwa wamejiunga na babu kumkamata Yule jogoo.

Tulikuwa tunasubiri chakula cha mchana, niliona hii kuwa fursa mufti kumwelezea babu kuwa nilikuwa na kusudi la kwenda naye mjini. Nilipomtamkia kuhusu kusudi langu, alicheka sana. Aliniambia, "Mji ni wenu nyinyi. Sisi watu wa shamba raha yetu ni kufukuzana na kazi hizi za sulubu. Kwenda kukaa mjini na nguvu zote hizi faida yake nini? Nasiskia siku hizi huko mjini kuna misongamano ya magari isiyoisha. Kuna haja gani kwenda kushinda kwenye gari kuharibu mda wako kwa sababu ya msongamano? Mimi hapa kwangu nikitaka kwenda kutekeleza shughuli zangu sipati kizuizi. Nakwenda tu".

"Sikiliza babu," nilimwambia", mji una raha zake. Wingi wa magari ni ishara ya maendeleo. Uwezo wa kifedha wa watu uko juu kuliko wa hapa kijijini. Leo hii mtu akipatwa na dharura ya ugonjwa hapa, kijiji kitafanya takilifu kumfikisha hospitalini. Mjini usafiri upo kila mahali wakati wote".

"Kule mjini mnadai kuuona mwanga na kuujua ustaarabu ila mumenoa," alisema babu, "maisha yenu afadhali ndege wavukao angani. Ni kama Ni kama mnavuka kutoka upande mmoja hadi mwingine, kana kwamba mnaendeshwa kwa nguvu za mtambo usioonekana. Jamaa hawajuani tena. Mizizi yenu hamuitambui. Mmekuwa mithili ya miti inayopendeza lakini isiyo na mizizi ya kutosha. Upepo hafifu uvumapo inalemewa na kujibwaga chini. Je, huo ndio

ustaarabu? Ustaarabu kwetu sisi watu wa kijijini ni mtu kuwaamkua wenziwe kila kukicha. Ni kujuliana hali. Ni kuombana. Kibaba cha unga au kibakuli cha mboga. Tunaishi tukijuana, si majina na sura tu, bali pia hata upishi wetu. Nyinyi mnaishi pasi na kujua majirani wenu. Je, wewe hukuona hata **kuku wangu hawa wanatangamana**?"

Swali hili lilipoachiliwa, nilihisi kama aliyetwikwa nanga. Kijasho chembamba kilinitoka. Kwa bahati nzuri meza ilikuwa imeshaandaliwa kipindi cha kupambana mezani kikawadia. Nilipokuwa nikila, nilitambua kitu kimoja, Yule kuku alikuwa na ladha ya kupendeza, tofauti na ile tuliyozoea kuwala kule mjini ila alikuwa mgumu kidogo. Nilipokuwa nikiwaza hili, nilisikia sauti ya babu tena.

"Chunga asikung'oe meno. Huyu ni kuku hasa. Atakusaidia kuimarisha meno. Hutakuwa na haja ya kwenda kumwona daktari wa meno. Sisi hapa kushiriki chakula kunatukumbusha kuwa kila shughuli ni kazi tosha. Hatuna muda wa kulaza damu". Alchukua bilauri ya mchuzi akapiga tama kisha akaendelea kuinyofua sima yake.

(a) Huku ukirejelea kifungu, faanua faida sita utakazopata ukiishi mashambani. (Alama 6)

(b) Eleza mitazamo ya wahusika wafuatao kuhusu mji;
- (i) Msimulizi (alama 3)
- (ii) Babu (alama 3)

(c) Andika maana za mafungu yafuatayo ya maneno kwa mujibu w taarifa. (alama 5)
- (i) Mawanda yake yaliyokula chumvi hadi yakakinai
- (ii) Kwenda kwa wakwe wako upate ndio wanakwenda uchi.
- (iii) Tulisalimiana huku tukipigiana pambaja.
- (iv) Raha yote ya kuwaona iligeuka karaha
- (v) Niliona kisunzi

(d) Taja na utoe mifano ya tamathali zozote 3 za fasihi zinazojitokeza katika kifungu hiki. (alama3)

**SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 50)**

3. (a) Tofautisha kimaana. (alama 2)
   - (i) Kipasuo
   - (ii) Kiyeyusho

   (b) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya wingi. (alama 2)
   Halati wa Maria huishi na mjomba.

   (c) Tunga sentensi ukitumia kiashiria kisisitizi cha mbali kidogo katika ngeli ya ki-vi umoja (alama 2)

   (d) Ainisha nomino katika sentensi ifuatayo.
   Kidani ambaye ni mwanariadha hodari alituzwa na baraza la mawaziri. (alama 3)

   (e) Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi 'ku' (alama 2)

   (f) Sahihisha;
   Shingo hili la ng'ombe hii ni refu mno. (alama 2)

   (g) Tunga sentensi iliyo na kiunganishi cha uteuzi. (alama 2)

   (h) Andika maneno yenye silabi zifuatazo; (alama 2)
      i. Konsonanti, konsonanti, irabu

   (i) Tunga sentensi yenye miundo ifuatayo: (alama 2)
   Kitenzi, kirai husishi.

(j) Tumia mchoro wa vingazi kuchanganua sentensi ifuatayo; (alama 3)
Sisi tunasoma lakini wao wamelala kabisa.

(k) Bainisha majukumu ya mofimu katika neno: walichokileta. (alama 3)

(l) Andika katika usemi halisi:
Kirima alisema angesomea mtihani huo siku hiyo jioni. (alama 2)

(m) Tunga sentensi moja moja kuonyesha matumizi mawili ya 'po' (alama 2)

(n) Kanusha:
Nimekuja kuomba msamaha. (alama 1)

4. (a) Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno: sita (alama 2)

(b) Mlo ufuatao hutumiwa wakati gani? (alama 1)

Kishuka ____________________________________________________________

(c) Tunaitaje? (alama 5)

(i) Sehemu ya nyumba ya ghorofa ambayo imetokeza nje.

(ii) Kupanda mbegu kwa kuzitawanya juu ya ardhi bila ya kupiga makuta.

Kifaa cha kutobolea mashimo kwenye mbao.

(iii) Wizara inayoshughulikia ujenzi na ukarabati wa barabara, forodha na reli.

(iv) Chombo cha kuangalia vitu vilivyo mbali.

(d) Andika kwa maneno: (alama 1)
2:55 alasiri

(e) Mnyama wa baharini mwenye mikia minane huitwa?

(f) Majira ya mvua nyingi ni masika, pia ni ________________________________ (alama 1)

(g) __________________________________ ni chombo kinachotumika kuchora maumbo mbalimbali. (alama 1)

(h) Vidudu vidogo vinavyoishi katika mwili wa kuku huitwa___________________________

(alama 1)

(i) Ni sayari gani iliyo na pete tatu na miezi 23? (alama 1)

(j) Andika maana ya methali: (alama 2)
Ulingo wa kwae haulindi manda

(k) Tegua kitendawili kifuatacho: (alama 1)
Gololi mbili zakwenda mbali

(l) Chai ya mkandaa ni rangi (alama 1)

(m) __________________________________________ ni uonjwa unaowashika watoto,

hukohoa sana na kutoa sauti kama ya fiimbi. (alama 1)

(n) Uchafu mweusi uletwao na moshi ni ________________________________ (alama 1)

5. **SEHEMU YA NNE: ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Eleza maana ya lugha sanifu. (alama 2)

(b) Fafanua mambo manne yanayochochea usanifishaji wa lugha. (alama 8)